# RIFT VALLEY SUPERIOR COLLAGE

Ni taasisi ya Elimu iliyojikita kutoa ufadhili wa masomo kwa vijana wa kitanzania ili waweze kujikwamua kiuchumi na kuwa msaada kwa familia zao na taifa kwa ujumla, Taasisi hii ilioanzishwa jijini Arusha kuanzia mwaka **2009** chini ya **SUPERIOR GUIDES& ACADEMIC LTD** ikisaidia kuwafundisha driver guides pekee wakati wa low session ikiongozwa na Mr.Elias Kapolondo na Mr.Elibariki Wellingtone Kitundu. Miaka kumi baadae **2019** taasisi hii ilihamishia ofisi zake Wilaya ya Monduli,Kata ya Migungani ambapo usimamizi wa Taasisi ulibaki kwa Elibariki Wellingtone Kitundu na kuwa chini ya **RIFT VALLEY SUPERIOR COLLAGE AND ACADEMIC LTD** baada ya mshirika mwenza kujiondoa kutokana na maradhi.

Taasisi iliendea kusaidia jamii ya kitanzania kwa kusaidia vijana katika fani za;

1. Hotel management.
2. Tourism and tour guide.
3. Hair dressing and beauty
4. Tailoring and
5. Nursey school teaching.
6. Computer studies.

Ambapo vijana wote wa kitanzania wanapata ufadhili wa masomo kwa asilimia 100% bila kulipia ada ya masomo isipokuwa wanalipa tu sare zao na malazi na mahafali tu. Kozi zote zinazotolewa hapa chuoni nikwa ngazi ya certificate nani kwa mwaka mmoja wenye semester mbili (2)kisha mahafali na baada ya hapo wanafunzi wanaenda kwenye mafunzo kwa vitendo kwa miezi mitatu(3).

**OFA ZITOLEWAZO CHUONI:**

- Lugha ya kiingereza Bure kwa wanafunzi wote.
- Lugha ya kifaransa Bure kwa wanafunzi wote.
- Intoduction to computer Bure kwa wanafunzi wote na
- Huduma ya mtandao Bure kabisa kwa wanafunzi wote **(FREE-WIFI).**

Taasisi hii ya Elimu iliyojikita kusaidia vijana kusoma bila kulipa ada ya masomo inashirikiana na marafiki wa ndani na nje kuwezesha uendeshaji na zaidi sana familia ya Mkurugenzi ndugu Elibariki Wellingtone Kitundu. Taasisi hii ya Elimu inapokea watu wote wa ndani na nje ya nchi ambao wako tayari kuwasaidia vijana kupata Elimu ya amali ili waweze kujikwamua kiuchumi na waweze kusaidia familia zao.

Misaada inayopokelewa ni pamoja na,

- fedha,
- chakula
- .mavazi,
- vitabu
- vifaa vya michezo pamoja na
- kutujengea Madarasa au Mabweni ili tuweze kusaidia vijana wengi zaidi kwa kila mwaka.

Taasisi hii ya Elimu ya Rift Valley mpaka sasa inauwezo wa kusaidia vijana 100 tu kwa mwaka ila kama tutapata watu wengi kutoka ndani na nje ya nchi watakaojitolea kulipia gharama ya sare na malazi kwa vijana tunatarajia kusaidia vijana wengi zaidi na ifikapo **2030** tunatarajia kuwa na uwezo wa kusaidia vijana **500** wa kitanzania kwa mwaka.

Taasisi hii pia inajihusisha na kupokea **watu wa kujitolea** kutoka ndani na nje ya nchi kufundisha vijana katika fani zote wanazojifunza pamoja na michezo na wanao jitolea kutoka nje ya nchi watalipia kiasi kidogo sana cha fedha kwaajili ya chakula na malazi.